**7 JUNI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 7 Juni, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

Na. 550

### Nafuu za Michango ya Kujiunga na Kidato cha Kwanza na Tano

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta unafuu wa gharama za michango ya kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza na cha tano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023 ambalo pamoja na mambo megine inatamka kuwa Serikali itahakikisha kuwa elimu ya awali, msingi na sekondari inatolewa bila ada katika mfumo wa umma. Aidha, Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2016 kuhusu utekelezaji wa Elimu Msingi Bila Malipo, unabainisha majukumu ya wadau wote ikiwa ni pamoja  na utaratibu wa kuzingatia ili kupata kibali cha mchango wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta unafuu wa gharama za michango, Serikali imetoa maelekezo ya kujiunga na kidato cha tano katika shule zote za sekondari za Serikali Tanzania ambapo ukomo wa michango hiyo umebainisha kuwa shilingi 80,000 kwa shule za bweni na shilingi 50,000 kwa shule za kutwa. Aidha, wanafunzi wa kidato cha kwanza wanapokelewa kwa kuzingatia Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2016 wa Elimu Msingi bila Ada ambapo wanafunzi hawatakiwi kutoa mchango wowote bila kibali cha Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Issa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ipo tayari kuainisha aina ya michango hiyo ambayo imeruhusiwa kuombewa kibali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali ipo tayari kutoa maelekezo kwa Wakuu wa Shule kuwaruhusu wanafunzi ambao hawana uwezo wa kuchangia michango hiyo kwa wakati? Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika,

ahsante, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi, Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2016 umeeleza na umeweka utaratibu wa kuzingatiwa ili kuweza kupata kibali kwa ajili ya kuwepo kwa michango katika shule za msingi lakini katika shule za sekondari iwapo kuna uhitaji na katika waraka huo ni lazima kupata kibali cha Mkuu wa Wilaya, lakini michango hii ambayo tunaizungumzia hapa inaweza ikawa ni ile michango ambayo wazazi wenyewe kupitia mikutano ya wazazi na kamati za shule wanakubaliana, kwa mfano wanaweza wakasema wanataka wanafunzi wawe wanavipindi vya ziada, kwa hiyo wanakubaliana kutoa michango ya aina fulani, lakini michango mingine ni hii ambayo inafahamika ambayo ni michango ya uendeshaji wa shule ambayo kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi ukomo umewekwa kwa shule za bweni kidato cha tano ni shilingi 80,000 na kwa shule za kutwa ni shilingi 50,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, naomba niendelee kusisitiza maagizo ambayo yametolewa huko awali kwamba Maafisa Elimu wa Mikoa, wa Wilaya, wa Kata, Wakuu wa Shule hawaruhusiwi kukataa kuwapokea wanafunzi kwa sababu tu wamekosa pesa za michango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nisisitize hilo kwa sababu ni maelekezo ambayo tayari yalishatolewa, mwanafunzi asikataliwe kupokelewa shuleni kwa sababu amekosa pesa ya michango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kutoa wito kwa wazazi wa wanafunzi wa kidato cha tano wale waliyochaguliwa kuingia kidato cha tano waweze kuhakikisha kwamba wanawapeleka watoto wao shule hata kama hawajakamilisha michango au kuwa na sare, ni muhimu sana watoto wanapochaguliwa kwenda kidato cha tano waweze kwenda shuleni kuripoti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri inatosha na ahsante. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

Na. 551

**Ukarabati Majengo Yaliyojengwa na MMEM**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kukarabati majengo yaliyojengwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu Msingi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilifanya tathimini ya mahitaji na hali ya miundombinu ya shule zote za msingi zikiwemo shule zenye majengo yaliyojengwa chini ya mpango wa maendeleo ya elimu msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2023/2024 Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ukarabati ambapo shilingi bilioni 70.39 zimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa shule 793.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukarabati wa shule chakavu zikiwemo shule zenye majengo yaliyojengwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu Msingi kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa madarasa mengi na nyumba za walimu nyingi zilizopo sasa hivi zilijengwa wakati wa mpango huu mkubwa wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM)

na kwa kuwa kiasi kinachotengwa sasa hivi kwenye halmashauri zetu kwa ajili ya ukarabati na ukamilishaji wa maboma ni kidogo; je, Serikali haioni haja ya kutafuta fedha nyingi ili madarasa haya ambayo yamechakaa yaweze kukarabatiwa kwa kiasi kikubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili mpango huu wa MMEM ulihusisha na uboreshaji na uendeshaji wa vituo vya walimu *(TRCs)*. Je, Serikali inampango gani wa kuendeleza vituo hivi ili walimu waweze kupata mafunzo kazini wakiwa katika maeneo yao ya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifanya kazi kubwa sana ya kufuatilia maslahi ya wananchi wake na hususani kwenye masuala pia ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa madarasa ambayo katika mwaka wa fedha 2022/2023 – 2023/2024 Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 70.39 kwa ajili ya ukarabati wa shule 793 lakini kupitia miradi ya elimu katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI miradi kutoka Wizarani, Serikali inatenga na imekuwa ikitoa fedha nyingi sana kwa ajili ya ukarabati wa shule zetu hizi kongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya shule hizi au ujenzi wa madarasa mapya unalenga kupunguza umbali wa wanafunzi kusafiri ili kufika mashuleni, lakini pia unalenga kupunguza msongamano.

Kwa hiyo, Serikali inaendelea kupitia mradi wa *BOOST* kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha inaendelea kukarabati shule kongwe, lakini kujenga madarasa mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusu vituo vya walimu naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia mradi wa *GPETSP,* mradi huu ambao upo kwenye awamu ya tatu umepanga kujenga vituo vya walimu 300 lakini mpaka hivi tunavyozungumza tayari kuna vituo vya walimu 252. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kutekeleza mradi huu na kuendelea kujenga vituo hivi muhimu vya walimu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shule ya Sekondari Ngonga iliyopo Wilayani Kyela imejengwa tangu mwaka 2007 mpaka sasa haina nyumba hata moja ya walimu; sasa je, Serikali ni lini itajenga nyumba za walimu kwenye shule hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mradi wa *GPETSP* nilioutaja hivi punde, mradi huu pia unalenga katika kujenga nyumba za walimu, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina mkakati na imetengeneza mipango ya kuhakikisha inaendelea kujenga nyumba za walimu katika maeneo mbalimbali nchini. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itakuja kufika ijenge nyumba za walimu katika shule aliyoitaja ya Ngonga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ipo tayari kuweka wazi mpango mkakati wa ukarabati shule kongwe zilizochakaa sana kwenye Wilaya ya Moshi Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imepanga kufanya ukarabati wa shule kongwe 50, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaweka katika kipaumbele ombi lake la kurekebishiwa au kufanyiwa marekebisho katika shule kongwe aliyoitaja katika jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve.

Na. 552

**Agizo kwa Halmashauri Kununua Viuadudu Kiwanda cha Kibaha**

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza: -

Je, Halmashauri ngapi zimetekeleza agizo la Waziri Mkuu kununua dawa za viuadudu kutoka Kiwanda cha Kibaha ili kutokomeza mazalia ya mbu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa afua ya unyunyuziaji wa viuadudu katika mazalia ya mbu yaliyotambuliwa katika halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuzielekeza halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kununua dawa za viuadudu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya halmashauri 126 zimetenga shilingi milioni 775.89 kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tweve.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema sijaridhika na majibu ya Serikali kwa sababu Serikali haijajibu swali langu la msingi. Mimi nilikuwa *very specific*, niliuliza ni halmashauri ngapi zimetekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu alilolifanya hapa Bungeni Mei, 2022 akiziagiza Serikali zote nchini, *I mean* halmashauri zote nchini ikiwepo hospitali za mkoa, kuhakikisha wanatenga bajeti na kwenda kununua dawa pale Kibaha na kupeleka kwenye halmashauri zetu nchini kuhakikisha wananyunyuzia mazalia ya mbu ili kuokoa maisha ya Watanzania ikiwemo wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kuna taratibu za kikanuni kama swali lako halijajibiwa unavyotaka Kanuni ya 53 unawajibu wa kufuatilia kanuni hiyo na ukajibiwa vingine.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Askofu Mathias Gwajima.

Na. 553

**Kudhibiti Mito Inayopanuka – Kawe**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa dharura wa kudhibiti mito inayopanuka na kuhatarisha maisha na mali za wananchi katika Jimbo la Kawe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto za mito kupanuka kutokana na mvua kubwa zilizonyesha. Serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali, kwanza, ni kutenga fedha

katika bajeti. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais imetenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu utakaowezesha ujenzi kwa maeneo yatakayopendekezwa kwa Mkoa wa Dar es salaam na Zanzibar. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kwa kushirikiana na Bonde la Wami-Ruvu tayari imeingia mkataba na kampuni ya *Meg Business Solution Limited* tokea tarehe 19 Aprili, 2024 kwa ajili ya kusafisha tope, taka ngumu na kudhibiti mmomonyoko wa kingo za Mto Mbezi eneo la Ukwamani, Mzimuni pamoja na ufukwe uliopo mtaa wa Mbezi A Kata ya Kawe. Hivyo, kwa kukamilika kwa kazi hizo kutachangia kudhibiti kupanuka kwa mto Mbezi katika kata ya Kawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa Serikali za Mitaa kote nchini kusimamia kikamilifu Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ili kuzuia shughuli za kibinadamu kama vile uchimbaji wa mchanga usiofuata utaratibu na kuelimisha jamii juu ya utunzaji wa mazingira ili kudhibiti upanukaji wa mito na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mito ya Nyakasangwe, Mbezi, Mpiji na Tegeta hiyo mito ni mito mikubwa na imeathiri sana familia zilizopo kule, nyumba zote zimebomoka, kwa mfano Mto Tegeta majumba yanaondoka, maji yamejaa kwenye maeneo ya wazi, watu wanashindwa kuishi vizuri na wanashambuliwa na magojwa kutokana na kujaa kwa maji hayo.

Je, Serikali sasa haioni kuna hatua gani za muda mfupi za kuliangali suala hili badala ya kusubiri hiyo bajeti ambayo inajumuisha maeneo kadhaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini sasa utaongozana na Mbunge wa Kawe Mheshimiwa Askofu Gwajima uende ukaone hali halisi ya Jimbo la Kawe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeeleza kwenye jibu letu la msingi, moja ni kwamba tumetenga fedha hizo na bahati nzuri tayari bajeti hii ndiyo inaendelea kumalizika, maana yake *once* tutakapopata fedha hizo tunakwenda kuanza huo upembuzi yakinifu, lakini kama nilivyoeleza tena kwenye jibu la msingi kwamba tayari tumeshaingia makubaliano na makubaliano haya yanakwenda kuanza haraka sana iwezekanavyo hapo mbele, ndani ya mwaka huu yanaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira, Serikali inatambua changamoto iliyokuwepo, inatambua wananchi wanapata shida lakini na sisi tupo mbioni kufanya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nimwambie Mheshimiwa Mbunge, nipo tayari kuhakikisha kwamba tunakwenda na tunafuatana pamoja tunakwenda Jimboni Kawe kwenda kuona hali ilivyo na kuona namna ya kuweza kuwasaidia wananchi, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Bagamoyo.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, katika Jimbo la Bagamoyo, Kata ya Mapinga maeneo ya Mingoi, Msongola, Kialaka na Kiembeni yamepata changamoto kubwa ya kupanuka kwa Mto Mpiji na kusababisha makazi ya watu kubomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali sasa itakuja kufanya tathimini, hatimaye kujenga kingo za mto huo ili maji yasiweze kuathiri nyumba za watu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi hili ambalo nimejibu sasa hivi hapa kwamba tayari tumeshatenga fedha shilingi bilioni moja, tunakwenda kuanza kufanya tathimini kwenye maeneo yote ambayo kwa namna moja ama nyingine yamepata athari ya mvua ama athari ya mabadiliko ya tabianchi ili tuone wapi tunahakikisha tunaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa baada ya Kawe tutakuja Bagamoyo kuja kuanza kufanya tathimini Mheshimiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Zacharia.

Na. 554

**Tathimini ya Mradi wa *REA* Mbulu Mjini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya upya tathimini ya maeneo kwenye Jimbo la Mbulu Mjini ambayo yalirukwa na Mradi wa *REA I* na *II*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbulu Mjini lina jumla ya vijiji 34, kati ya hivyo, vijiji 31 vimepatiwa umeme na vijiji vitatu vilivyosalia yaani Kwam, Aicho na Tsawa vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA III* Mzunguko wa II ambapo kazi imeshaanza

na inatarajia kukamilika tarehe 30 Juni, 2024. Aidha, Jimbo la Mbulu Mjini lina mitaa 58 ambapo mitaa 46 imepatiwa umeme na mitaa 12 haina umeme. Kutokana na tathmini iliyofanywa na *REA*, mitaa 12 iliyosalia itapatiwa umeme kupitia mradi mkubwa wa kupeleka umeme vitongojini ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2024/2025 kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa majibu yake.

Kwa kuwa maeneo yote ya mitaa iliyotajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri maeneo mengi makazi ya watu yamerukwa na uingizaji wa umeme; je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati mwafaka wa kuingiza yale maeneo ya huduma ya afya, elimu na maeneo ya makanisa kuingizwa kwenye mradi huu wa kuingiza umeme kwa shilingi 27,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tayari katika eneo la Mbulu Mjini, maeneo mengi yaliyopelekewa huduma ya umeme yamekuwa na changamoto nyingi ya wananchi kushindwa kuingiza umeme kwa yale yaliyofikiwa.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka kutazama upya nchi nzima maeneo yote ambayo wananchi wameshindwa kuingiza umeme kwa gharama kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kwanza, kwenye upande wa maeneo ambayo yamepitiwa na umeme, lakini taasisi hazina umeme, tayari nimeshajibu kwenye jibu la msingi kwamba, mitaa ile 12 iliyobakia tunao mkakati wa kupelekea umeme kupitia mradi wa vitongoji kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwasihi *REA* waweze kufanya tathmini kwenye maeneo haya na kuweza kuona kama maeneo haya yanaweza yakaingizwa kwenye Mradi wa *Peri Urban* na kisha taasisi zilizopo katika maeneo haya na yenyewe yaweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, kwenye maeneo yenye sura ya vijiji lakini yapo mijini tayari Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO)* tumeshafanya mapitio kwenye maeneo 1,570 ya maeneo ambayo yana sura ya vijiji, lakini yapo mijini ili kuweza kuona uwezekano wa kutoka shilingi 320,000 hadi shilingi 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, maeneo yake ambayo yana picha hiyo na yenyewe tutayapitia kuweza kuona kama yanakidhi vigezo vya kuingia kwenye utaratibu huu wa shilingi 27,000. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Katika Jimbo la Tarime Vijijini maeneo ya Vijiji vya Nyangoto, Kerende, Mjini Kati, Nyabichune na Nyamwaga wananchi wangu wanalipia umeme shilingi 320,000 kinyume na sera ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kauli ya Serikali wananchi wapate umeme kwa bei nafuu ambayo imeelekezwa vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo haya ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge, tutayapitia kuona kama yapo kwenye yale maeneo 1,570 ambayo tumeshayaainisha na kama hayapo tutayafanyia tathmini kuweza kuona kama na yenyewe yanaweza kuingia katika mpango huo ili wananchi waweze kupata huduma ya kuunganisha umeme kwa shilingi 27,000. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itawapatia umeme wananchi waliopo katika Mtaa wa Msisina, Msalagala na Kisowele, Iringa Mjini kwa sababu maeneo hayo yalikuwa katika Jimbo la Ismani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mitaa hii ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge ya Msisina, Msalagala na Kisowele itaenda kupatiwa umeme kupitia mwaka wa fedha 2024/2025. Ofisi yetu ya *TANESCO* - Mkoa wa Iringa, imeshaweka kwenye mpango huo, lakini vilevile katika mitaa hiyo kuna Mtaa mmoja pia wa Kipululu na wenyewe hauna umeme. Tulishawaelekeza *TANESCO* kupitia Ofisi ya Mkoa waweze kutenga *special fund* ili mitaa yote hii minne ambayo haina umeme waweze kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mitaa hii tayari ipo kwenye mpango na yote itapata umeme kwa mwaka ujao wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Londo kwa niaba ya Mheshimiwa Gulamali.

Na. 555

**Ujenzi wa *VETA* Choma**

**MHE. DENNIS L. LONDO K.n.y. MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, Serikali itawaunga mkono *World Vision* kuendeleza ujenzi wa Chuo cha *VETA* Choma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua juhudi za wadau mbalimbali katika kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi nchini ikiwemo *Word Vision* ambao pamoja na juhudi zingine wanendelea na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* kinachojengwa katika Wilaya ya Igunga. Aidha, Serikali inaendelea na azma yake ya kuhakikisha kila Wilaya nchini inakuwa na Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imekamilisha ujenzi wa Vyuo 25 vya *VETA* vya Wilaya pamoja na vyuo vinne vya *VETA* vya Mikoa ambapo Wilaya ya Igunga ambayo *World Vision* inaendelea na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi ni miongoni mwa Wilaya zilizojengewa vyuo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari kuunga mkono juhudi hizo na imeshaelekeza Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* kutembelea chuo hicho na kuwasilisha maeneo yanayopendekezwa Serikali iunge mkono ili chuo hiki kiweze kukamilika na kuanza kutoa mafunzo kama ilivyopangwa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi binafsi zimekuwa wadau wakubwa katika suala zima la elimu ya ufundi na kuna uwekezaji mkubwa, je, Serikali haioni wakati umefika sasa wa kuwa na mikataba na waendeshaji wa vyuo hivi kama ilivyo hospitali binafsi kwenye mkataba wa *DHH? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Wilaya ya Kilosa ilitoa kwa makusudi Chuo cha *VETA* pale Mikumi kwa Serikali na toka nimekabidhi hakuna ukarabati wowote ambao umefanyika mpaka sasa; je, Serikali haioni wakati umefika sasa wa kurudisha chuo hiki kwa halmashauri ambayo ni miliki wa awali baada ya Serikali kushindwa kuwekeza chochote? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Mheshimiwa Mbunge, anatoa ushauri kwamba, kwa nini sasa Serikali haioni umuhimu wa kuingia mikataba ya ubia juu ya uendeshaji wa vyuo hivi? Kwa vile huu ni ushauri ambao Mheshimiwa Mbunge anatupa kama Serikali, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ushauri wake tumeupokea tutakwenda kuufanyia tathmini ya kina ili kuweza kuona maeneo gani ambayo Serikali inaweza ikaingia ubia pamoja na mashirika binafsi katika uendeshaji wa vyuo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili, kuhusiana na Chuo hiki cha Mikumi nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge tumepeleka fedha katika mwaka uliopita wa fedha pale kwa ajili ya kufanya ukarabati, lakini na katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 tumetenga fedha kwa ajili ya kuendelea na ukarabati pamoja na uongezaji wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mwakani 2024/2025 tumetenga fedha kwenye bajeti yetu kuhakikisha kwamba vyuo vyote vile vya zamani ambavyo tulivichukua kutoka kwa taasisi binafsi pamoja na halmashauri vinaenda kukarabatiwa, kuongezewa majengo, lakini vilevile kupeleka watumishi na vifaa kwa ajili ya mafunzo kwa vijana wetu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga *VETA* kila Wilaya sambamba na hilo, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa vijana wanaosoma *VETA* mikopo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, safari ni hatua na tulishaanza utoaji wa mikopo kwanza kwa vijana wetu ambao walikuwa wanasoma elimu ya juu, lakini mwaka uliopita tumeanza kutoa mikopo katika elimu ya kati na kwa vile tunaendelea na utaratibu huu kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha tunaweza tukafikia katika maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imeshafanya kazi kubwa sana kwenye eneo hili la mafunzo ya *VETA,* kwa sababu ada ya vijana hawa au ada ya mafunzo kwa wale wanafunzi wa kutwa ni shilingi 60,000 na wale wanafunzi wa bweni ni shilingi 120,000. Serikali inachangia ruzuku kwa kila mwanafunzi zaidi ya shilingi 1,150,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa ruzuku hii na tutaangalia vilevile uwezekano wa kuweza kutoa mikopo katika kada hii muhimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa hii nafasi, je, ni lini ujenzi wa Chuo cha *VETA* kinachojengwa Kata ya Uwiro, Arumeru Mashariki utamalizika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nikiri kwamba kuna ujenzi ambao unaendelea katika Jimbo la Mheshimiwa Pallangyo, kule Arumeru na mimi mwenyewe nimeshafanya ziara zaidi ya mara mbili kwenye eneo lile kuangalia maendeleo ya chuo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, malengo yetu ni kuhakikisha kwamba mpaka kufika mwezi Oktoba, mwaka huu vyuo hivi katika awamu ya kwanza

viwe vimekamilika ili mwezi wa Novemba tuweze kuanza kutoa zile kozi za muda mfupi na Januari mwakani tuweze kuanza kutoa zile kozi za muda mrefu.

Kwa hiyo, hayo ndio malengo yetu tutahakikisha kwamba, ifikapo mwezi Oktoba, vyuo hivi vimekamilika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Ngonyani. *(Makofi)*

Na. 556

**Kuboresha Viwanda vya Uzalishaji wa Vyakula vya Mifugo Nchini**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha viwanda vya uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini vikiwemo viwanda vya vyakula vya mifugo ambavyo vingi vinatumia malighafi za kilimo kama vile mahindi, soya na mashudu ya alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kutoka tani 1,380,000 mwaka 2021/2022 hadi tani 1,580,000 mwaka 2022/2023. Aidha, viwanda vipya 22 vya kuzalisha vyakula vya mifugo vimesajiliwa katika mikoa nane kwa maana ya Arusha vinne, Kilimanjaro vitatu, Dar es Salaam vinne, Morogoro viwili, Iringa vitatu, Mbeya kimoja, Pwani vitatu na Shinyanga viwili na hivyo kufanya viwanda vya kuzalisha vyakula vya mifugo kuongezeka kutoka 199 mwaka 2021/2022 hadi 221 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya uzalishaji wa vyakula vya mifugo na kuhakikisha kuwa vyakula vinavyozalishwa vinakuwa na viwango stahiki kulingana na mahitaji ya mifugo husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuruhusu vyakula kutoka nje kuingizwa ndani ya nchi?

(b) Kwa kuwa chakula cha mifugo ni ghali sana jambo ambalo limekuwa ni changamoto sana kwa wafugaji; je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi kwa uingizaji wa vyakula hivyo ikiwa pamoja na kupunguza tozo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Msongozi kwa ufuatiliaji kuhusiana na sekta hii ya mifugo hasa vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tumekuwa na changamoto ya vyakula vya mifugo vinavyozalishwa kwa maana ya kusindikwa hapa nchini ukiacha vile vya kawaida kwa maana ya nyasi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tuna nakisi kubwa ya uzalishaji wa vyakula vya mifugo katika viwanda vyetu na hasa katika maeneo mengine. Ni 55% tu ya vyakula vingi vinavyozalishwa kwenye sekta hii katika kulisha mifugo kwa maana ya kuku, lakini maeneo mengine bado tuna changamoto hiyo.

Kwa hiyo, mpaka sasa tayari Serikali inaruhusu vyakula vingi vilivyosindikwa kwa ajili ya mifugo vinaagizwa kutoka nje. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya hivyo, lakini jitihada ni kuona tunazalisha sisi wenyewe ndani. Kwa hiyo, tayari hilo tunalifanya, kwa sababu tuna nakisi hiyo ya vyakula vya mifugo vinavyosindikwa katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na la pili, ni kweli tuna haja na tunaendelea kutoa vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi kwenye viwanda vinavyozalisha vyakula vya mifugo kwa sababu kama nilivyosema asilimia zaidi ya 60 tunaagiza kutoka nje.

Kwa hiyo, Serikali tunaendelea kuweka mipango Madhubuti ya kusaidia viwanda vya ndani na kutoa vivutio zaidi kwa wale wanaoingiza kwa sasa, lakini pia kwa wale wanaozalisha kwenye viwanda vyetu vya ndani, kwa sababu ndio haja kubwa kuona vyakula hivi vinasindikwa katika nchi yetu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Chege.

Na. 557

**Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Miji 28 - Rorya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Mradi wa Maji wa Miji 28 utaanza kutekelezwa katika Wilaya ya Rorya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Rorya - Tarime kwa kutumia chanzo cha maji ya Ziwa Victoria. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* yenye uwezo wa kuzalisha

maji lita milioni 29 kwa siku, ujenzi wa miundombinu ya kutibu maji *(water treatment plant)* yenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 28 kwa siku, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 110, ujenzi wa kituo cha kusukuma maji *(booster station)* pamoja na ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 12.5% na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2025 na utanufaisha wakazi wapatao 460,885 waishio kwenye Wilaya za Rorya, Tarime pamoja na Mji wa Sirari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, mradi huu ndio kwanza, upo 12.5% kwa maana yake upo nyuma kulingana na muda wa kimkataba mpaka sasa na sisi wananchi wa Rorya huu ndio mradi ambao ni suluhisho kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nipate *commitment* ya Serikali, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri mradi huu utakamilika na kuanza kutoa maji Halmashauri ya Wilaya ya Rorya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Mradi wa Bukura, Gabimori, Sakawa pamoja na Nyihara ni miradi ambayo imesimama kwa muda mrefu. Ninataka nijue, Mheshimiwa Waziri na imesimama, kwa sababu ya changamoto ya kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini fedha zitakwenda kwa ajili ya uendelezaji na ukamilifu wa miradi hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi mradi huu utakamilika Julai, 2025 na mpaka sasa tuna takribani miezi 12 ambayo imebaki. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa sababu najua kwamba mradi huu ni wa kimkakati katika eneo lake na kwa kisiasa na kwa afya ya wananchi wake. Tunamhakikishia kwamba pesa zitaendelea kupelekwa ili mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali la pili, maeneo ya Bukura, Sakawa, Nyihara ambapo najua Nyihara ndio Mheshimiwa Mbunge anapotoka, tunatambua kwamba miradi hii inaenda kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Mbunge atupatie ushirikiano na wananchi wake kipindi ambacho tutaanza utekelezaji ambapo ni baada ya mwezi Julai, maana yake kwamba sasa wananchi wataendelea kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini sasa Serikali au mna mkakati gani wa kubadilisha mabomba ya zamani kuweka mapya katika Jimbo la Temeke, kwa sababu mabomba haya yanapopasuka kunakuwa na upotevu mkubwa wa maji, lakini pia uharibifu wa nyumba za watu katika eneo ambalo mabomba hayo yamepasuka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa mabomba chakavu yanatusababishia Serikali upotevu wa maji. Tunapozalisha maji kwa mfano lita 1,000,000 na unakuta kwamba upotevu ni 40% maana yake kwamba ile *production cost* inaishia kwenye gharama ambazo anapelekewa mwananchi wakati maji yanayofika yanakuwa hayatoshi. Kwa hiyo, Serikali ina mkakati wa kuhakisha kwamba tunaendelea kupitia miundombinu yetu

ambayo tayari imeshakuwa chakavu ili kuhakikisha kwamba tumeendelea kuibadilisha kwa kadiri fedha ambavyo tunakuwa tunapata ili kuhakikisha kwamba, upotevu wa maji angalau tunaendana na upotevu unaokubalika Kimataifa ambayo ni 15%.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutalifanyia kazi katika maeneo ya Temeke kuhakikisha kwamba wananchi wa Temeke hawapati changamoto ya maji kusambaa mitaani na wanapata maji ya uhakika ambayo ni toshelezi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nikushukuru Naibu Waziri kwa ziara ya kibabe uliyoifanya katika Jimbo la Kilolo. *(Makofi)*

Sasa swali langu la nyongeza Mradi wa Maji wa Masege, Masalali na Kihesa Mgagao umeanza kusua sua kutokana na mkandarasi kutokulipwa kwa wakati; je, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi ili mradi ule uweze kukamilika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya na kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwa kuendelea kutupatia ushirikiano na sisi tunajiona kwamba tuna mwakilishi wa wananchi ambaye anahitaji kuwasemea wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge katika mradi huo ambao kama ambavyo umedai unasuasua Serikali kupitia Wizara ya Maji tumekaa na wenzetu Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba, sasa wakandarasi wetu ambao wanatekeleza mradi huo walipwe pesa ili wahakikishe kwamba mradi huo unakamilika kwa wakati na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi; Mheshimiwa Naibu Waziri upatikanaji wa maji Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyere ni 52% na upotevu wa maji ni 47%, tunahitaji shilingi milioni 400 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini watatupatia hizo fedha tuweze kukarabati miundombinu iliyoharibika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwia Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni swali ambalo tayari Serikali tulilijibu hapa Bungeni na tayari Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso alielekeza fedha shilingi milioni 400 zipelekwe kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, mradi huu unakamilika. Mradi huo unapokamilika wananchi wa Namanyere wanapata huduma ya maji safi na salama, lakini vilevile unaenda kusaidia kuhakikisha kwamba, miundombinu yetu inaboreshwa na kuepusha upotevu wa maji ambao ni hasara kubwa kwa Serikali.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kushirikiana na tutahakikisha kwamba, fedha hizo zinafika kwa wakati na mradi uendelee kutekelezwa. Tunakupongeza kwa kuendelea kufanya kazi vizuri na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na utekelezaji wa Ilani ya CCM inaendelea kutekelezwa vizuri sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Mwanyika.

Na. 558

**Hitaji la Maji Kijiji cha Mtila – Njombe Mjini**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, ni lini wananchi wa Kijiji cha Mtila Kata ya Matola Njombe Mjini watapelekewa maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma ya maji katika Kijiji cha Mtila Kata ya Matola Njombe Mjini, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetenga fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi pamoja na kuchimba kisima kirefu ili kupata chanzo cha maji. Aidha, baada ya kupatikana kwa chanzo hicho cha maji Serikali itafanya usanifu wa miundombinu ya usambazaji maji kwa ajili ya kunufaisha wananchi wa Kijiji cha Mtila, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kuhusiana na suala la Mtila nawatakia heri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza yanayohusiana na mradi mwingine wa Igongwi. Mradi muhimu sana wa kimkakati.

Swali la kwanza, mradi huu ambao utapeleka maji kwenye kata tatu na vijiji zaidi ya nane umekuwa ukisuasua, lakini tunajua umefikia 80% na kilichosababisha usikamilike kwa miaka saba ni fedha kutolewa kidogo kidogo. Swali, Serikali haioni sasa ni muda mwafaka wa kutoa fedha zote ili angalau hii 20% iliyobakia ikamilike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mradi huu hata fedha zote zikitolewa unaweza usikamilike kwa sababu maji yanatoka kwenye Milima ya Madope katika Wilaya ya Ludewa na yanapita Kijiji cha Luvuyo ambapo wananchi nao wanataka mradi wao ukamilike ili waruhusu maji haya yaende Njombe.

Sasa Serikali ina mkakati gani kuhakikisha maji kwenye Kijiji cha Luvuyo ambapo wananchi wamezuia yasipite wanapata fedha ili mradi wao nao ukamilike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali kama ifuatavyo; natambua Mheshimiwa Mwanyika mradi huu kwake ni mradi wa kimkakati lakini napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba mradi huu ni mradi wa kimkakati wa Chama Cha Mapinduzi na ni mradi wa kimkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi ya kimkakati zaidi ya nane na miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, nyingine ipo katika 15%, 50% na 60% lakini kwa bahati nzuri kabisa mradi huu umeshafika katika 80% na bado 20%. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na sisi tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaendelea kupeleka fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapeleka fedha kulingana na upatikanaji wake kwa sababu miradi hii yote mikubwa inahitaji fedha nyingi sana na tunatamani sana Watanzania wote katika miradi hii ambayo tunaitekeleza, yote iweze kukamilika waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kupeleka fedha kulingana na namna ambavyo mkandarasi atakuwa analeta hati za madai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili naomba nilipokee kwa ajili ya kuwaelekeza wataalamu ili wakafanye tathmini na kujiridhisha kwamba kijiji hicho kitapata maji kutoka kwenye chanzo kipi na tukishajiridhisha basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaweza kupeleka fedha kama ambavyo ameomba kwa sababu yeye ndiyo msemaji, yeye ndiye mwakilishi wa Mheshimiwa Rais katika jimbo lake, sisi tutahakikisha kwamba tunamuunga mkono kwa kuhakikisha tunapeleka pesa kulingana na tathmini ambayo itakuwa imefanywa na wataalamu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kuna ahadi ya muda mrefu ya kupeleka maji katika Kata ya Mnazi katika Vijiji vya Langoni A, Langoni B, Kwemkwazu pamoja na Kiwanja. Ni lini Serikali itakamilisha usanifu na ujenzi wa mradi huu wa maji katika kata hii ya kimkakati kabisa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo, Mheshimiwa Shangazi huu mradi na hasa Kata ya Mnazi natambua kabisa kwamba Serikali kupitia Wizara ya Maji tuna ahadi ya kufika katika kata hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafika katika kata hii na kuhakikisha kwamba tunasukuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tayari Serikali imeshapata mtaalamu mshauri na gharama ya mradi ya takribani shilingi milioni 800 na tayari mtaalamu mshauri huyu ameshakabidhiwa *site* kwa ajili ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mtaalamu wetu atakapokamilika basi tunaamini kwamba mkandarasi atapatikana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa kwa haraka iwezekanavyo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliopo Jukwaa la Spika, mgeni wa Mheshimiwa Spika, Ndugu Leonard Kwihaya, Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa. *(Makofi)*

Wageni kumi wa Naibu Spika ambao Wahadhiri kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM);* Dkt. Siriel Mchembe, Ndugu Juma Maira, Dkt. Bernadetha Rushahu, Ndugu Marie Kigalu, Ndugu Aurelia Kimaro, Mhandisi Mtatiro Boniphace Marwa, Ndugu Mohamed Seif, Ndugu Ambwene Stephen Kajula, Dkt. Chisuligwe Salum Khadudu na Dkt. Mtunga Mabula. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Naibu Spika, Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi Kata ya Upanga Mashariki na Seneti ya Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu Josephine Bulengero - Mwenyekiti wa CCM Kata ya Upanga Mashariki, Ndugu James Mwely - Katibu wa CCM Kata ya Upanga Mashariki, Ndugu Arafa Kiula -Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Upanga Mashariki, Ndugu Mohammed Bawaziri - Mwenyekit wa CCM Kata ya Jangwani, Ndugu Pascrates Albinus -Mwenyekiti wa Seneti na Ndugu Mabula Mabula - Katibu wa Seneti. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Naibu Spika ni *Tulia Marathon* Jimbo la Ilala. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa William Lukuvi na Wabunge wote wa Mkoa wa Iringa ambao Wajumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Iringa, Ndugu Daudi Yassin Mlowe - Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Ndugu Said Goha - Katibu wa CCM Mkoa, Ndugu Zainabu Mwamwindi - Mwenyekiti wa UWT Mkoa, Ndugu Agrey Tonga - Mwenyekiti UVCCM Mkoa, Ndugu Fadhil Ngajiro - Mwenyekiti wa Wazazi Mkoa, Ndugu Joseph Ryata - Katibu Siasa na Uenezi Mkoa, Ndugu Lucia Sulle - Katibu wa UWT Mkoa, Ndugu Anitha Magelanga - Kaimu Katibu wa Wazazi Mkoa, Ndugu Aisha Mpuya - Katibu wa UVCCM Mkoa, Ndugu Dickson Mwaipopo – Mjumbe, Ndugu Tumaini Msowoya – Mjumbe na Ndugu Seki Kasuga – Mjumbe. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine 77 wa Naibu Spika, Umoja wa wanariadha wa Jimbo la Ilala, Walezi wa Seneti, Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi, Mwenyekiti na Katibu wa Machinga Wilaya ya Ilala, na *Ilala Timamu Unit Development Association (ITUDA)* Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii naye ni mwalimu, mtunzi na mwimbaji wa nyimbo za injili kutoka Mkinga Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mwandishi wa Habari kutoka Redio Safina Arusha. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, mwananchi kutoka Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, walimu kutoka Shule za Halmashauri ya Mji wa Geita. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Wanakwaya wa Kanisa la Anglikana kutoka Kata ya Namwanga Jimbo la Lulindi, Masasi Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Umoja wa Kikristo wa Wanafunzi Tanzania Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wageni 83 wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Viongozi wa Umoja wa Wanafunzi wa Kikristo Tanzania kutoka Mufindi, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Ndugu Agnes Kanyonyi, Mstaafu wa Shirika la Wakimbizi Duniani *(UNHCR)* na *Sister (Sr.)* Jasinta Paulo kutoka Jimbo Katoliki Bukoba ambaye anafanya Kazi katika Kituo cha Malezi Kashozi. *(Makofi)*

Wapo pia watumishi wawili kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 56 na walimu nane wa Shule *ya St. Andrew Kijenge* kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 58 na walimu watano wa Shule ya Msingi *Holy Cross* kutoka Kilosa, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 wa Shule ya Msingi Lucky Vincent ya Jijini Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Norah Mzeru.

Na. 559

**Serikali Kuwawezesha Wadau wa Michezo Kuzalisha Vipaji**

**MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wadau wa michezo kuwekeza katika kuzalisha vipaji vya michezo mbalimbali hasa mpira wa miguu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kuwawezesha wadau wake kuwekeza katika kuzalisha vipaji vya michezo hususan mpira wa miguu ikiwemo kuandaa miongozo na kanuni mahususi zinazowalinda wadau wanaoanzisha shule maalumu za kukuza na kuendeleza vipaji vya michezo *(sports academies)* ili kuhakikisha wananufaishwa na uwekezaji wanaoufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua kadhaa nyingine, Serikali inawaunganisha wadau hao na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania kupitia programu kadhaa za kuibua na kuendeleza vipaji zikiwemo UMITASHUMTA, UMISETA na UMISAVUTA. Aidha, Serikali imeanzisha mafunzo ya elimu ya michezo ngazi za Astashahada na Stashahada katika vyuo sita nchini vikiwemo Vyuo vya Ualimu Butimba, Korogwe, Mpwapwa, Monduli na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Hali kadhalika, Serikali inaendelea kuimarisha utoaji wa mafunzo ya shahada ya kwanza katika elimu ya michezo kwenye Chuo Kikuu

cha Dar es Salaam kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu wa kufundisha michezo ili kupunguza gharama za uwekezaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mzeru.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kujenga na kuboresha viwanja vya michezo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu je, Serikali imejipangaje kuendeleza vipaji vya vijana hao? *(Makofi)*

Swali la pili, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kuboresha viwanja vya michezo mashuleni na kwenye vyuo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Norah kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, mpango wa Serikali kuendeleza vipaji, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Serikali kwa kushirikiana na *TFF* tunaandaa mashindano mbalimbali ya vijana ili vipaji ambavyo vimeweza kupatikana viweze kukuzwa na kuendelezwa kupitia mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kuna ligi ya *under 17,* lengo ni kuonesha vipaji hivyo vinakuwa vipi, tuna UMISETA na UMITASHUMTA ambayo kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu ataenda kufungua kule Tabora. Mashindano hayo yote yana lengo la kuhakikisha kwamba vipaji vinavyopatikana vinaweza kuendelezwa. Katika kituo cha *TFF* Tanga na Dar es salaam mafunzo ya kuendeleza vipaji hivyo yanaendelea na hata hivi

sasa ninavyoongea wataalamu wapo wanatoa mafunzo hayo. Kwa hiyo, tunahakikisha vipaji hivyo vitaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili, katika bajeti tuliyopitisha mwaka huu tarehe 23 Mei, tulisema Serikali ina mpango wa kujenga shule 56 ili kuzibadilisha kuwa shule za michezo. Shule hizo 56 ambazo zitakuwa ni shule mbili katika kila mkoa Tanzania Bara na Visiwani zitakuwa ni mahususi kwa kuchukua vipaji hivyo na kuviendeleza, lakini kuendeleza miundombinu ya michezo katika mashule hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, moja kati ya wadau wakubwa wa michezo ni Serikali na Serikali ina shule zake za sekondari na za msingi wanafunzi wengi hawana vifaa vya michezo.

Je, Wizara haioni sababu ya kuwa na mkakati wa makusudi wa kuwasiliana na Wizara ya Fedha mkashusha kodi kwenye vifaa vya michezo shuleni ili ku-*support* watoto wapate vifaa vya michezo kwa sababu imekuwa ni changamoto kubwa kwenye Taifa letu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Festo Sanga kwa ufuatiliaji mzuri wa maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Serikali kwa kushirikiana na *TFF* tumegawa mipira 1,000 kwa ajili ya wanafunzi katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani. Tumepokea wazo lake, tutaongea na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba tunatoa au kupunguza kodi katika vifaa vya michezo ili vijana hao wengi na Watanzania kwa ujumla waweze kumudu vifaa hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimefurahi kusikia kwamba Tanzania tuna ligi ya *under 17* lakini ligi hii haionekani kuwa *promoted*.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kuvitaka vilabu vya *premier league* kulazimishwa kuwa na timu za *under 17* ambazo zinashiriki katika hiyo *premier league?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas kwa mchango wake kuendeleza michezo. Nilimwona akishangilia kombe lile la Yanga hivi juzi, lakini ningemwomba pia angeshangilia na lile la Simba la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la msingi, ligi ya *under 17* inaendeshwa na vilabu vya *championship, league under 20* inaendeshwa na vilabu vya *premier league* lakini nimepokea wazo lake kwamba vilabu vya *premier league* sasa navyo viwe na *league* ya *under 17* na *league* ya *under 14* katika mkakati wa kukuza na kuibua vipaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwani Mheshimiwa Tarimba hujui kama Simba tayari wanayo timu ya *under 17*? Kaa chini Mheshimiwa Tarimba. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna Mheshimiwa Asia, tunaendelea na Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Kachauka.

**MHE. ZUBERI M. KACHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo au Maji? Naomba swali langu namba…

**NAIBU SPIKA:** Ngoja ngoja Mheshimiwa Kuchauka subiri.

Tunaenda Wizara ya Habari na Mawasiliano, Mheshimiwa Mkundi.

Na. 560

**Kuongeza Nguvu ya Mnara na Kupatiwa *Generator* - Kata ya Bukiko**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza nguvu ya mnara katika Kata ya Bukiko kutoka *2G* hadi *3G* na kuweka *generator* kwa kuwa kata hiyo ina shida kubwa ya mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* itaijumuisha kata ya Bukiko katika mradi wa kuboresha huduma za mawasiliano kwa kuongeza teknolojia za *3G* na *4G* na pia mradi huu utaimarisha miundombinu ya nishati ikiwemo ya kuweka *generator*. Utekelezaji wa mradi huu utaanza katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa bajeti ya kazi hii ilitengwa kwenye mwaka wa fedha 2022/2023 lakini utekelezaji wake umekuwa unasogezwa mbele kila wakati, Serikali haiona kwamba inakwamisha maendeleo ya wananchi wa Kata hii ya Bukiko?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa changamoto za mawasiliano kwenye Jimbo la Ukerewe zipo maeneo mengi, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kufanya ziara Jimboni Ukerewe ili upate uhalisia wa changamoto hizi na

kupata ufumbuzi wa kitaalamu wa uhakika kwa ajili ya matatizo haya? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Mkundi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kukamilisha maendeleo naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa Ukerewe, Serikali haiwezi kukwamisha maendeleo, imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kupitia mnara uliopo na naomba nikupe uhakika kazi hii inakwenda kuimarishwa mwaka ujao wa fedha na tutaisimamia pamoja mimi na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kufanya ziara Mheshimiwa Mbunge ni wajibu wangu, hakuna shida baada ya hapa tuonane tuweze kupanga ratiba ya pamoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu ya Tigo ilishinda zabuni ya kutengeneza mnara wa mawasiliano ya simu katika Kata ya Uru Shimbwe, lakini kazi hii ni kama vile haijaanza; je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inasimamia utekelezaji wa mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndakidemi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze amekuwa akifuatilia hili na nitoe tu wito kwa makampuni yote ambayo

yamepewa kazi, tunahitaji kuona kazi zinafanyika kwa wakati na nitasimamia hili mimi mwenyewe Mheshimiwa Mbunge usipate shaka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata ya Gehandu kwa sasa wanatumia mnara wa mawasiliano uliopo Kata ya Ishiponga. Je, ni lini Serikali itapeleka mnara wa mawasiliano katika Kata ya Gehandu kwa sababu huu wa Ishiponga katika Jimbo la Hanang unasuasua? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asia Halamga na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili eneo la Gehandu tayari tunalifanyia kazi, kwanza, kuboresha ule mnara wa jirani kwa sababu masuala ya mawasiliano ni suala la *signals* kufika. Kwa hiyo, tutaongezea vifaa ili kuona *signals* zinaweza kufika vizuri zaidi wakati tunajipanga kujenga mnara mpya katika eneo hili la Gehandu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Ilima, Jimbo la Rungwe, Kijiji cha Katundulu kuna shida kubwa sana ya usikivu wa minara ya simu; ni lini Serikali mtatuletea mnara katika kijiji kile? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hili eneo la Ilima tayari lipo katika mpango wa Wizara. Napenda kukutoa hofu tunakwenda kujenga mnara, lakini vilevile kuhakikisha tunaongezea vifaa katika minara ya jirani ili *signals* ziweze kufika Ilima na maeneo yote yale ya jirani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Kuchauka.

Na. 561

**Kuchunguza Ugonjwa Unaoikumba Mikorosho – Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kuleta wataalamu Liwale kufanya utafiti kujua chanzo cha ugonjwa wa majani ya mikorosho kunyauka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeanza kufanya utafiti wa kina ili kutambua chanzo cha ugonjwa majani kunyauka unaoikumba mikorosho katika Wilaya ya Liwale. Utafiti huo ulianza kufanyika mwaka 2023 na wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania kupitia Kituo cha *TARI* Naliendele kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya awali ya utafiti huo yamebaini kuwa chanzo cha mnyauko wa majani ya mikorosho katika Wilaya ya Liwale ni fangasi aina ya *Fusarium oxysporum f.*

sp na ikajulikana kuwa ni kimelea kinachoishi kwenye udongo ambacho husababisha ugonjwa wa mnyauko fusari *(fusarium wilt)* na ugonjwa huu ni tishio kwa kuwa unasababisha kukauka kwa mikorosho. Serikali imeanza kutoa elimu kwa wakulima na wataalamu wa kilimo kuhusu mbinu za awali za kukabiliana na ugonjwa huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna aina nyingi sana ya viuatilifu madukani ukiacha vile viuatilifu ambavyo vinatolewa ruzuku na Serikali, lakini kwenye aduka kuna viuatilifu vingi sana ambavyo zinachanganya wakulima na kupunguza uzalishaji wa mazao haya ya korosho. Je, Serikali ina mkakati gani wa kufuatilia kuhakikisha viuatilifu vinavyopatikana kwenye maduka hayo vyote vina ubora unaofanana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wapo wasafirishaji waliosafirisha pembejeo zile za ruzuku kutoka kwenye Vyama vyetu Vikuu kwenda kwenye Vyama vya Msingi. Leo ni mwaka mzima sasa hivi hawajalipwa na tayari benki wameanza kuwafilisi. Nini kauli ya Serikali kuwasaidia wasafirishaji wale ili kuwapatia fedha zao wakalipa kwenye madeni Serikalini na benki? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, jambo la kwanza, nampongeza vilevile Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia mambo makubwa ya msingi katika sekta ya kilimo. Nimwondoe shaka tu kwamba, tunatambuka kwamba kuna viuatilifu vingi katika maduka, lakini viuatilifu karibu vyote kabla havijaingia katika maduka tuna mamlaka zetu nchini ikiwemo *TPHPA* pamoja na *TBS* ambazo zimekuwa zikithibitisha ubora wake na kila wakati tumekuwa tukifanya *control* kwa kupitia na kukagua. Kwa hiyo, tutaendelea kulifuatilia hili ili

kuhakikisha kwamba vigezo vyote na masharti yanazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wasafirishaji hususani wa zao la korosho, ninaiagiza Bodi ya Korosho kuhakikisha kwamba kabla hatujafunga mwisho wa mwaka huu wa fedha wawe wamewalipa wasafirishaji hawa kwa ajili ya kuondokana na madeni ambayo wamekuwa nayo katika benki, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo Jimboni Liwale linafanana na tatizo lililopo katika baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Dodoma, mimea ya mahindi ilikauka katika msimu huu. Nini kauli ya Serikali kutokana na kadhia hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba changamoto yoyote inapotokea sisi Wizara ya Kilimo kupitia mamlaka yetu ya utafiti *TARI* huwa tunaiagiza kwenye eneo husika na kufanya tafiti ili kugundua ukubwa wa tatizo ama tatizo limetokana na nini na kilichotokea Dodoma, tulishaiagiza *TARI* na inaendelea na utafiti, wakishamaliza tutaleta matokeo na tutamjulisha Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, mikorosho imekuwa ikikumbwa na magonjwa mengi na inaonekana kama yameshindwa kutibika; je, Serikali sasa iko tayari kushirikiana na watafiti ikiwezekana hata wa kutoka nje ya nchi ili kutatua changamoto hiyo ya magonjwa na kuongeza tija kwa wakulima ambao wamekuwa wakilima lakini wanapata tija ndogo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Serikali tuko tayari kushirikiana na mdau yeyote kuja kufanya tafiti hapa nchini awe anatoka nje ya nchi au taasisi yoyote ndani ya nchi tuko tayari kufanya nao lakini kwa kuzingatia masharti na sheria za nchi yetu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Francis Ndulane.

Na. 562

**Hitaji la Mbegu Bora za Ufuta – Wilaya ya Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itawapatia mbegu bora za ufuta wananchi wa Wilaya ya Kilwa waweze kuzalisha ufuta mwingi kwani wanatumia mbegu za asili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuwahamasisha wakulima wa zao la ufuta katika Wilaya ya Kilwa kutumia mbegu bora ili kuongeza uzalishaji. Katika msimu wa mwaka 2023/2024 Serikali ilisambaza bure jumla ya tani 10 za mbegu bora ya ufuta kwa wakulima wa Kilwa na kuweka mashamba ya mfano ya kilimo bora cha ufuta katika Kata za Likawage na Mandawa. Aidha, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI)* imetoa elimu kwa wakulima katika Kata za Miguruwe na Mandawa kuhusu umuhimu wa matumizi ya mbegu bora na kanuni za kilimo bora cha zao la ufuta ili kuongeza tija. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, zao hili la ufuta katika Wilaya ya Kilwa limekuwa likikabiliwa sana na changamoto ya wadudu waharibifu pamoja na kukosa dawa; je, Serikali ina mkakati gani wa kukakikisha kwamba inapeleka dawa za kuua wadudu katika zao hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kufuatia kuwepo kwa mvua kubwa za *El–Nino* na Kimbunga Hidaya, mazao ya minazi na michungwa yapatayo 100,000 yamezolewa na mafuriko; je, Serikali ina mkakati gani wa kusaidia wakulima wa mazao haya ya minazi na michungwa ili kuhakikisha kwamba tunarudisha mazao haya katika uzalishaji wa kawaida? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimpongeze Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kwa kuendelea kuwafuatilia kwa karibu wananchi wake hususani wanaoji-*engage* katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja namthibitishia tu kwamba panapotokea uharibifu wowote, moja ya jukumu letu sisi kama Wizara ni kuleta dawa ama viuatilifu kwa ajili ya kuondoa hiyo changamoto ya mazao ambayo itakuwa imewapata. Kwa hiyo, tunachohitaji tu ni kupewa taarifa kutoka katika halmashauri husika ama mkoa husika na sisi tutafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, tuko tayari muda wowote kutekeleza jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu minazi ambayo imechukuliwa, nakuthibitishia tu kwamba kabla ya mwezi wa kumi mwaka huu Wizara tutasambaza minazi bure kwa wananchi ambao walikutwa na adha hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda Wizara ya Madini, Mheshimiwa Agnes Hokororo kwa niaba ya Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Na. 563

**Uchimbaji wa Mbunyu Kata ya Chiwata – Ndanda**

**MHE. AGNES E. HOKORORO K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha uchimbaji wa Mbunyu unatekelezwa katika Kata ya Chiwata - Ndanda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini ilitoa leseni mbili za uchimbaji wa kati zenye namba ML 591/2018 na ML 592/2018 kwa Kampuni ya *Volt Graphite Tanzania Public Limited* ili kuendesha shughuli za uchimbaji wa madini ya kinywe *(graphite)* katika Mradi wa Mbunyu katika Jimbo la Ndanda. Hata hivyo, mradi haukuanza shughuli za uchimbaji tangu kutolewa kwa leseni hizo kutokana na kuchelewa kwa makubaliano kati ya Kampuni hiyo ya *Volt Graphite* na wanunuzi *(off-takers)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kwa sasa mwekezaji amesaini mkataba na Kampuni ya *Property Matrix Limited* kwa ajili ya kufanya tathmini ya ulipaji fidia kwa wananchi waliopo katika eneo la mradi. Aidha, Kampuni ya *Volt Graphite* ipo katika majadiliano ya mwisho na wanunuzi *(off-takers)* wa *graphite* ili kuruhusu kuanza kwa ujenzi wa kiwanda cha kuongeza thamani madini hayo, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu ulikusudiwa uanze tangu mwaka 2016 lakini mpaka sasa hivi taratibu zimechelewa kama alivyojibu kwenye majibu ya msingi. Je, ni lini mradi huu utaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, vijiji vinavyonufaika na mradi huo wa Mbunyu, Chiwata na Chidya, vitanufaikaje kutokana na mradi huo utakapoanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la kwanza, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema katika majibu ya swali la msingi, sasa hivi *off-takers* wale wanunuzi wa hiyo *graphite* ambayo ni kati ya madini mkakati yanayohitajika sasa hivi duniani kwa utengenezaji wa *battery* na vifaa vya magari yasiyotumia mafuta, yanatumia umeme, ni kwamba wamepatikana wawekezaji hao kutoka Marekani na kutoka Ulaya na wako katika hatua za mwisho ili uzalishaji uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa swali lake la pili, faida za mradi huu utakapoanza ni nyingi, kwanza ninawapongeza hawa ndugu zetu wa *Volt Graphite* kwa sababu hata kabla mradi huu haujaanza, katika upande wa kutoa mchango kwa jamii, wameshachangia fedha katika ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Kijiji cha Nangwale, lakini pia wanachangia posho za walimu wawili wa kujitolea katika shule iliyoko katika kijiji hicho kama sehemu ya kuonesha dhamira yao njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wameanzisha ofisi mbili katika Kijiji hicho cha Nangwale na Chiwata ambazo zinadumisha mahusiano na jamii ile. Ila watakapoanza kanuni zetu zinawataka kupitia kanuni za uwajibikaji na ushiriki wa Watanzania *(local content)* watoe ajira na wawaruhusu wenyeji na Watanzania

kutoa huduma zote muhimu ambazo wanaweza kuzitoa pamoja na *CSR* sasa ambao wameanza kutoa kabla ya mradi kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mradi huu utakuwa na manufaa makubwa na ninawaasa wananchi wa maeneo hayo ya Mradi wa Mbunyu wakae mkao wa kutoa ushirikiano katika kampuni hii ambapo itakapoanza uzalishaji, matunda yake yatasambaa katika jamii husika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, wananchi wa Kijiji cha Mpepo kwa muda mrefu hawajaweza kuendelea na shughuli zao kutokana na suala kwamba kuna mwekezaji ilikuwa aendeleze eneo hilo kwa ajili ya uchimbaji na awalipe fidia, lakini imechukua muda mrefu sasa huyu mwekezaji hajaweza kufanya hiyo.

Je, Mheshimiwa Waziri utalichukua hili ili uweze kulifuatilia ili wananchi hawa waweze kuendelea na shughuli zao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Niabu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wawekezaji kuchelewesha fidia na kusababisha wananchi kutoweza kuendeleza yale maeneo ni suala ambalo linasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016 ambayo inamtaka aliyefanya uthamini ili afidie watu ndani ya miezi sita aanze kuwalipa na asipowalipa alipe fidia kwa kipindi cha miaka miwili na asipolipa uthamini huo unakufa na unaanza upya.

Kwa hiyo, hao wananchi wa Mpepo ambao wamekwamishwa kuendelea na uendelezaji wa maeneo yao kama uthamini umechewa kulipwa na miaka miwili imeshapita, huo uthamini hauna maana tena ina maana utafanywa upya na *commitment* ya huyu kuendelea na uthamini aweze kuwekeza, sisi kama Wizara tutafuatilia ili tujue kikwazo ni nini na ikibidi sasa

aanze uthamini upya ili wananchi wafidiwe ili mradi huo uweze kuendelea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge Bungeni asubuhi hii; kuna wageni wa Mheshimiwa Mrisho Gambo, wanafunzi 100 na walimu kumi kutoka Shule ya Msingi Lucky Vincent ya Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, maveterani wanaokuja kucheza na Waheshimiwa Wabunge tarehe 8 Juni, 2024, karibuni. *(Makofi)*

Kuna wageni waliotembelea Mbunge kwa ajili ya mafunzo; wageni 13 ambao ni familia ya Ndugu Josephine Kulwa kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo tarehe 07 Juni kutakuwa na semina kuhusu usalama wa viongozi katika eneo la Bunge itakayofanyika saa 8.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake, Mheshimiwa Shally Raymond anaomba kuwatangazia Wabunge wanawake kuwa leo tarehe 7 Juni, mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge saa nne asubuhi kutakuwa na Kongamano litakalofanyika katika Ukumbi wa Mabeyo.

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho Jumamosi tarehe 8 Juni kutakuwa na semina itakayohusu uchambuzi wa bajeti kwa kuzingatia masuala ya jinsia *(Gender responsive budget)* itakayofanyika saa 3.00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hii ya mafunzo inaratibiwa kupitia Mradi wetu wa Kulijengea Bunge Uwezo wa *LSP III. (Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho Jumamosi tarehe 8 Juni kutakuwa na semina kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 pamoja Kanuni zake itakayotolewa na Wizara ya Fedha. Semina hii itafanyika saa 6.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni kipindi cha Waheshimiwa Wabunge kurudi kwenye Kamati zenu na kuendelea na mijadala ya Kamati na masuala ya bajeti.

Sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.16 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 10 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*